

www.shepherdserve.org

Unaruhusiwa kuchapa, kunakili, kugawa au kusambaza haya kwa njia yoyote ile, mradi tu usibadili chochote wala kukata chochote. Vile vile hairuhusiwi kuuza maelezo haya. © Haki zote zimehifadhiwa 2006 David Servant

Mchungaji Afanyaye Watu Kuwa Wanafunzi

David Servant

Sura Ya Kumi Na Moja Ubatizo Wa Roho Mtakatifu

Mtu anaposoma kitabu cha Matendo ya Mitume, utendaji wa Roho Mtakatifu katika kanisa la kwanza ni dhahiri kwenye kila ukurasa. Ukiiondoa kazi ya Roho Mtakatifu katika kitabu cha Matendo, huna kitu kilichobaki. Kweli, aliwitia nguvu wanafunzi wa kwanza ili “kuupindua ulimwengu” (tazama Matendo 17:6).

Siku hizi katika dunia yetu, mahali ambapo kanisa linakua kwa haraka ni pale ambapo wafuasi wa Yesu wmejitoa kwa Roho Mtakatifu kabisa na kuwezeshwa Naye. Hili lisitushangaze. Roho Mtakatifu anaweza kufanikisha mambo mengi kwa muda wa nukta kumi kuliko tunayoweza kufanikisha sisi kwa muda wa miaka elfu kumi, kwa juhudini zetu. Kwa hiyo, ni kitu muhimu sana kwamba mtumishi anayefanya watu kuwa wanafunzi aelewé Maandiko yanafundisha nini juu ya kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha na huduma za waamini.

Mara kwa mara katika kitabu cha Matendo ya Mitume tunapata mifano ya waamini wakibatizwa kwa Roho Mtakatifu na kuwezeshwa kufanya huduma. Tuwe na busara kujifunza somo hili ili ikiwezekana, hata sisi tupate walichopata na kufurahia msaada wa kimuujiza waliopata wao kutoka kwa Roho Mtakatifu. Ingawa kuna wanaodai kwamba matendo hayo ya miujiza ya Roho Mtakatifu ilikuwa ni kwa ajili ya wakati wa mitume wenyewe tu, mimi sipati hoja ya kiMaandiko, kihistoria wala ya kiakili, yenyé kuunga mkono maoni hayo. Wale wanaoamini kinachoahidiwa katika Neno la Mungu watapata baraka zilizotajwa. Sawa na Waisraeli ambao hawakuamini, walioshindwa kuingia katika Nchi ya Ahadi, wale wasioamini ahadi za Mungu kwa leo watashindwa kuingia katika yote ambayo Mungu amewaandalia. Je, wewe uko kundi gani? Mimi niko miongoni mwa wenyewe kuamini!

Kazi Mbili Za Roho Mtakatifu

Kila mtaaliyemwamini Bwana Yesu Kristo kabisa amefanyiwa kazi na Roho Mtakatifu maishani mwake. Utu wake wa ndani – au roho – umezaliwa upya kwa Roho Mtakatifu (ona Tito 3:5), na Roho Mtakatifu anaka andani yake (ona Warumi 8:9; 1Wakor. 6:19). Yeye “amezaliwa kwa Roho” (Yohana 3:5).

Kwa kutoelea hili, Wakristo wengi wa Pentekoste na Karizmatiki wamekosea kwa kuwaambia waamini fulani kwamba hawakuwa na Roho Mtakatifu kama hawakuwa

wamebatizwa kwa Roho Mtakat ifu na kunena kwa lugha. Hili ni kosa kutokana na Maandiko na hata ujuzi halisi wa maisha. Waamini wengi wasiokuwa WaPentekoste au WaKarizmatiki wana ushuhuda zaidi kwamba Roho anakaa ndani yao kuliko baadhi ya waamini wa KiPentekoste au KiKarizmatiki! Wanaonyesha matunda ya Roho yaliyotajwa na Paulo katika Wagalatia 5:22-23 kwa kiwango kikubwa sana, kitu ambacho kisingewezekana bila kuwa na Roho Mtakatifu ndani.

Kwa kuwa tu mtu *amezaliwa* na Roho si uhakikisho kwamba *amebatizwa* pia kwa Roho Mtakatifu. Kulingana na Biblia, kuzaliwa na Roho Mtakatifu na kubatizwa kwa Roho Mtakatifu ni vitu viwili tofauti.

Tunapoanza kuchambua mada hii, hebu kwanza tutazame yale ambayo Yesu aliyasema wakati fulani kuhusu Roho Mtakatifu, kwa mwanamke asiyeokoka, huko kisimani Samaria.

Kama ungelijjua karama ya Mungu naye ni nani akuambiaye, ‘Nipe maji ninywe’, ungalimwomba yeze naye angelikupa maji yaliyo hai. ... Kila anywaye maji haya [kutoka kisimani] ataona kiu tena; walakini yeote atakayekunyuwa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele (Yohana 4:10, 13-14).

Ni halali kufikiri kwamba yale maji yanayokaa ndani ya mtu ambayo Yesu alizungumzia ni Roho Mtakatifu, anayekaa ndani ya wale wanaoamini. Baadaye katika Injili ya Yohana, Yesu alitumia tena maneno “maji yaliyo hai”, na hapo hakuna shaka kwamba alikuwa anazungumza juu ya Roho Mtakatifu.

Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikuu, Yesu akasimama na kupaza sauti yake, akasema hivi: ‘Mtu akiona kiu na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.’ Na *neno hilo alilisema kwa habari ya Roho*, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa (Yohana 7:37-39, TLR. Maneno *mepesi* kukazia).

Hapa, Yesu hakuzungumza juu ya maji yaliyo hai kuwa “chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele”. Badala yake, hayo maji yaliyo hai yanafanyika *mito* ibubujikayo kutoka ndani ya mwenye kupokea.

Mafungu haya mawili ya Maandiko kutoka Injili ya Yohana huonyesha vizuri sana tofauti kati ya kuzaliwa kwa Roho na kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Kuzaliwa kwa Roho ni kwa faida ya yule aliyezaliwa upya, ili aweze kufurahia uzima wa milele. Mtu anapozaliwa tena kwa Roho, anapata hifadhi ya Roho ndani yake yenye kumpa uzima wa milele.

Lakini kubatizwa kwa Roho Mtakatifu ni kwa faida ya wengine, maana inawawezesha waamini kuwashudumia watu wengine kwa nguvu za Roho. “Mito ya maji yaliyo hai” itabubujika kutoka ndani yao, ikileta baraka za Mungu kwa wengine kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

Ubatizo Wa Roho Mtakatifu Unahitajika Kwa Nini?

Tunahitaji sana msaada wa Roho Mtakatifu ili tuweze kuwahudumia wengine! Bila msaada Wake, hatuwezi kutumaini kuwafanya watu wote kuwa wanafunzi. Hiyo ndiyo sababu hasa iliyomfanya Yesu kuahidi kuwabatiza waamini kwa Roho Mtakatifu – ili dunia ipate kusikia Injili. Aliwaambia hivi wanafunzi Wake:

Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu, lakini kaeni humu mjini hata *mvikwe uwezo* utokao juu (Luka 24:49 – Maneno mepesi kutilia mkazo).

Luka tena anaandika maneno mengine ya Yesu, kwamba:

Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyyoweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini *mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu*, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi (Matendo 1:7-8. Maneno mepesi kutilia mkazo).

Yesu aliwaambia wanafunzi Wake hata wasiondoke Yerusalem mpaka “wavikwe uwezo kutoka juu.” Alijua wasingekuwa na uwezo kama si hivyo, na wangeshindwa kabisa kutekeleza kazi aliyokuwa amewapa. Tunaona kwamba mara baada ya kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, Mungu alianza kuwatumia wao kwa njia ya ajabu sana kueneza Injili.

Wakristo milioni nyingi duniani, baada ya kubatizwa na Roho Mtakatifu, wamefahamu na kutambua kiwango kipy cha nguvu, hasa wakati wa kuwashuhudia watu ambao hawajaokoka. Waligundua kwamba maneno yao yalikuwa na maana zaidi, na kwamba wakati mwingine walitaja maandiko ambayo hawakujua waliyafahamu. Baadhi yao walijikuta wenyewe wakiwa wameitwa na kupewa karama kwa ajili ya huduma fulani, kama vile uinjilisti. Wengine waligundua kwamba Mungu aliwatumia kama alivyopenda katika karama mbalimbali za Roho Mtakatifu. Ujuzi wao ni wa KiBiblia kabisa. Wale wanaopinga ujuzi wao hawana msingi wowote KiBiblia kwa ajili ya kuwapinga. Ukweli ni kwamba wanapingana na Mungu.

Isitushangaze sisi ambao tumeitwa kumwiga Kristo kwamba tumeitwa kuiga ujuzi Wake na ROho Mtakatifu. Yeye alitungwa mimba tumboni mwa Mariamu kwa Roho Mtakatifu (ona Mathayo 1:20). Yeye aliyezaliwa kwa Roho alikuja kubatizwa na Roho kabla ya kuanza huduma Yake (ona Mathayo 3:16). Kama Yesu alihitaji kubatizwa na Roho Mtakatifu ili kumwezesha katika huduma, sisi je?

Ushahidi Wa Kwanza Kwamba Mtu Amebatizwa Katika Roho Mtakatifu

Mwamini anapobatizwa katika Roho Mtakatifu, ushahidi wa kwanza wa ujuzi wake ni kwamba ananena kwa lugha mpya, au kama Maandiko yanavyosema wakati mwingine, “lugha nyingine.” Kuna maandiko mengi sana yanayothibitisha jambo hilo. Hebu tuyatazame.

Kwanza – Muda mfupi tu kabla ya kupaa Kwake, yesu alisema kwamba mojawapo ya ishara zitakazofuatana na waamini ni kwamba wangesema kwa lugha mpya.

Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa. *Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio*: kwa jina langu watatoa pepo, *watasema kwa lugha mpya* (Marko 16:15-17. Maneno mepesi kutilia mkazo).

Kuna waandishi wa vitabu vya mafafanuzi vya Biblia wanaodai kwamba maandiko hayo hayapaswi kuwa katika Biblia zetu kwa sababu baadhi ya magombo fulani ya zamani ya Agano Jipyä hayana fungu hilo. Lakini, mengi katika magombo ya kale yana fungu hilo, na hakuna tafsiri nyingi za Kiswahili za Biblia ambazo hazina fungu hilo. Tena, yale ambayo Yesu alisema katika maandiko haya yanalingana vizuri tuna ujuzi wa kanisa la kwanza kama tunavyopata habari zake katika kitabu cha Matendo ya Mitume.

Kuna mifano mitano katika kitabu cha Matendo, yenyé kuonyesha waamini wakibatizwa kwa mara ya kwanza na Roho Mtakatifu. Hebu tuitazame yote, na tutakapokuwa tunafanya hivyo, tutajiuliza maswali mawili yafuatayo: (1) Je, Ubatizo kwa Roho Mtakatifu ulikuwa ni kitu baada ya wokovu? Na (2) Je, waliopokea walinena kwa lugha mpya? Hii itatusaidia kuelewa mapenzi ya Mungu kwa ajili ya waamini siku za leo.

Yerusalem

Mfano wa kwanza unapatikana katika Matendo sura ya 2, wakati wale wanafunzi mia na ishirini walipobatizwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste.

Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upemo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. *Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka* (Matendo 2:1-4. Maneno mepesi kutilia mkazo).

Hakuna shaka yoyote kwamba wale waamini mia na ishirini walikuwa wamekwisha okoka na kuzaliwa mara ya pili kabla ya wakati huo. Basi, walipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu baada ya wokovu. Hata hivyo isingewezekana kwao kubatizwa katika Roho Mtakatifu kabla ya wakati huo kwa sababu Roho Mtakatifu hakuwa ametolewa kwa kanisa kabla ya siku hiyo.

Ni dhahiri basi kwamba ishara iliyoambatana na tendo hilo ilikuwa kunena kwa lugha nyingine.

Samaria

Mfano wa pili wa waamini kubatizwa kwa Roho Mtakatifu unapatikana katika Matendo sura ya 8, wakati Filipo alipokwenda jijini Samaria na kuhubiri Injili huko.

Lakini [WaSamaria] walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake. ... Na mitume waliokuwako Yerusalem waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana, ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu, kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu (Matendo 8:12-16).

Ni wazi kwamba Wakristo WaSamaria walipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kama kitu cha zaidi baada ya wokovu wao. Biblia inasema wazi kabisa kwamba kabla Petro na Yohana hawajafika, WaSamaria tayari walikuwa “wamelipokea neno la Mungu,” wameiamini Injili na kubatizwa katika maji. Lakini, wakati Petro na Yohana walipokuja kuwaombea, Maandiko yanasema ni ili wampokee Roho Mtakatifu.” Iwekwe wazi zaidi kuliko hapo jamani?

Je, waamini wa Samaria walinenen kwa lugha mpya walipobatizwa kwa Roho Mtakatifu? Biblia haisemi, lakini inasema kwamba kitu cha kushangaza kilitokea kwao. Wakati mtu aitwaye Simoni alipoona yaliyotokea baada ya Petro na Yohana kuweka mikono yao juu ya Wakristo wa Samaria, alijaribu kununua kutoka kwao uwezo huo huo wa kumtoa Roho Mtakatifu.

Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, ‘Nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemweka mikono yangu apokee Roho Mtakatifu’ (Matendo 8:17-19).

Je, Simoni aliona nini kilichomshika hivyo? Tayari alikwisha ona miujiza mingi tu mingine, kama vile watu wakitolewa mapepo na waliolemaa na viwete wakiponywa (ona Matendo 8:6-7). Yeye mwenyewe alikuwa amehusika katika uchawi hapo kwanza, akiwashangaza watu wote wa Samaria (ona Matendo 8:9-10). Kama ni hivyo, alichokiona wakati Petro na Yohana walipoomba lazima kingekuwa kitu cha ajabu sana. Ingawa hatuwezi kusema kwa uhakika kabisa, inaonekana ni sawa kufikiri kwamba aliona kitu cha kushangaza kile kile kilichokuwa kinatokea kila mara ambapo Wakristo walipokea Roho Mtakatifu katika kitabu cha Matendo ya Mitume – aliona na kuwasikia watu wa Samaria wakinena kwa lugha nyingine.

Sauli Huko Dameski

Mara ya tatu katika kitabu cha Matendo kunapotajwa mtu akimpokea Roho Mtakatifu ni kwa habari ya Sauli wa Tarso, ambaye baadaye alijulikana kama mtume Paulo. Aliokolewa akiwa njiani kwenda Dameski, na alikuwa amepofuka kwa muda. Siku tatu baada ya kuokoka kwake, mtu aitwaye Anania alitumwa kwake na Mungu.

Anania akaenda zake, akaingia mle nyumbani, akamwekeea mikono akisema, ‘Ndugu Sauli! Bwana amenituma, Yesu, yeye aliyekutokea katika njia ulioijia, upate kuona tena, ukajazwe Roho Mtakatifu.’ Mara

vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama, akabatizwa (Matendo 9:17, 18).

Hapana shaka kwamba Sauli aliokoka kabla ya Anania kufika kumwombea. Alimwamini Bwana Yesu alipokuwa yungali njiani kwenda Dameski, na mara moja akatii maagizo ya Bwana wake mpya. Tena, wakati Anania alipokutana na Sauli mara ya kwanza alimwita “*Ndugu Sauli*.” Ona kwamba Anania alimwambia Sauli kwamba amekuja ili apate kuona *na* kujazwa na Roho Mtakatifu. Basi kwa Sauli, kujazwa na Roho Mtakatifu – au kubatizwa basi – kulitokea siku tatu tu baada ya kuokoka kwake.

Maandiko hayasemi tukio hilo la Sauli kubatizwa na Roho Mtakatifu, lakini bila shaka lilifanyika muda mfupi tu baada ya Anania kufika mahali Sauli alipokuwa. Hakuna shaka kwamba Sauli alinena kwa lugha kwa sababu, baadaye anasema katika 1Wakor. 14:18 hivi: “Namshukuru Mungu kwamba mimi nanena kwa lugha kuliko ninyi wote” (TLR).

Kaisaria

Mara ya nne ambapo waamini wanatajwa kwamba wamebatizwa kwa Roho Mtakatifu ni katika Matendo 10. Mtume Petro alikuwa ameagizwa na Mungu kwenda kuhubiri Injili huko Kaisaria, nyumbani kwa Kornelio. Mara tu baada ya Petro kudhihirisha kwamba wokovu hupokelewa kwa imani katika Yesu, wasikilizaji wake wote waliokuwa si Wayahudi (yaani, WaMataifa) waliitikia kwa imani, na Roho Mtakatifu akawashukia.

Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akajibu, ‘Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi?’ Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo (Matendo 10:44-48a).

Hapa, inaonekana kwamba watu wote wa nyumbani mwa Kornelio, waliokuwa wasiokuwa Wayahudi wa kwanza kumwamini Yesu, walizaliwa mara ya pili na kubatizwa hapo hapo.

Tukijifunza maandiko yanayoambatana na hayo pamoja na mantiki kihistoria, kuna sababu iliyodhahiri kabisa iliyomfanya Mungu asingojee Petro na waamini wenzake wawawekee mikono waamini wale wasiokuwa Wayahudi, ili wapokee Roho Mtakatifu. Petro na waamini wanzake wa Kiyahudi walikuwa na shida sana kuamini kwamba wasiokuwa Wayahudi wanaweza kuokoka – achilia mbali kumpokea Roho Mtakatifu! Yawezekana wasingewaombea familia ya Kornelio wapokee ubatizo wa Roho Mtakatifu. Basi Mungu akafanya kwa enzi Yake. Mungua likuwa anamfundisha Petro na wenzake kitu kuhusu neema Yake ya ajabu kwa wasiokuwa Wayahudi.

Kilichomshawishi Petro na wale waamini wengine Wayahudi kwamba familia ya Kornelio walipokea Roho Mtakatifu kweli ni nini? Luka anaandika hivi: “Kwa maana

waliwasikia wakisema kwa lugha” (Luka 10:46). Petro akatamka kwamba wasiokuwa Wayahudi wamempokea Roho Mtakatifu kama wale mia na ishirini walivyofanya siku ya Pentekoste (ona 10:47).

Efeso

Mara ya tano ambapo waamini wanatajwa kubatizwa katika Roho Mtakatifu ni katika Matendo sura ya 19. Alipokuwa anasafiri na kupitia Efeso, mtume Paulo alikutana na wanafunzi fulani, akawauliza hivi: “Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?” (Matendo 19:2, TLR).

Paulo, mtu aliyeandika sehemu kubwa ya nyaraka za Agano Jipyä aliamini dhahiri kabisa kwamba inawezekana kumpokea Yesu na usiwe umempokea Roho Mtakatifu. Vinginevyo, asingeuliza swali alilouliza.

Wale ndugu wakajibu kwamba hawakuwa hata wamesikia kuhusu Roho Mtakatifu. Ni kwamba walikuwa wamesikia kuhusu Masiye anayekuja tu kupitia Yohana Mbatizaji, ambaye alikuwa amewabatiza. Paulo mara moja akawabatiza tena kwa maji, na wakati huu wakawa wamebatizwa Kikristo. Hatimaye, Paulo akawawekea mikono ili wapokee Roho Mtakatifu.

Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu. Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao, wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri. Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili (Matendo 19:5-7).

Hapa tena ni kitu wazi kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa baada ya wokovu, bila kujali kama hao watu kumi na mbili walikuwa wameokoka kabla ya kukutana na Paulo. Tena, ishara iliyoambatana na wao kubatizwa kwa Roho Mtakatifu ilikuwa kunena kwa lugha (na hapa, kutabiri pia).

Sawa

Hebu tuitazame tena ile mifano mitano. Katika mifano minne, ubatizo kwa Roho Mtakatifu ulikuwa kitu kilichotokea baada ya wokovu.

Katika mifano mitatu, Maandiko yanasema wazi kabisa kwamba wahusika walinena kwa lugha nyingine. Tena, Paulo alipokutana na Anania, yeche kubatizwa kwa Roho Mtakatifu hakuelezwii, lakini tunajua kwamba hatimaye alikuja kunena kwa lugha. Huo ni mfano wa nne.

Katika mfano uliosalia, kitu kisicho cha kawaida kilitokea wakati waamini huko Samaria walipompokea Roho Mtakatifu kwa sababu, Simoni alijaribu kununua nguvu za kumtoa Roho Mtakatifu.

Basi, ushahidi uko wazi kabisa. Katika kanisa la kwanza, waamini waliozaliwa mara ya pili walipata kitu kingine na Roho Mtakatifu, na walipofanya hivyo, walinena kwa lugha nyingine. Hii isitushangaze kwa sababu Yesu alisema wale wanaomwamini watanena kwa lugha nyingine.

Tunao ushahidi thabiti kabisa kwamba kila mtu aliyezaliwa mara ya pili anatakiwa pia kupokea kazi nyingine ya Roho Mtakatifu – kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Tena, kila mwamini anapaswa kutazamia kunena kwa lugha nyingine wakati anapobatizwa kwa Roho Mtakatifu.

Jinsi Ya Kupokea Ubatizo Wa Roho Mtakatifu

Roho Mtakatifu hupokelewa kwa imani (Wagal. 3:5), sawa tu na zawadi nyingine zote za Mungu. Ili kuwa na imani ya kupokea, mwamini anatakiwa kwanza ashawishike kwamba ni mapenzi ya Mungu kwake kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Kama ana mashaka au wasiwasi, hatapokea (ona Yakobo 1:6-7).

Hakuna mwamini yejote mwenye sababu nzuri ya kuamini kwamba si mapenzi ya Mungu kwake kupokea Roho Mtakatifu, kwa sababu Yesu alieleza waziwazi mapenzi ya Mungu kuhusu swala hilo.

Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao? (Luka 11:13).

Ahadi hiyo kutoka kwa Yesu inapaswa kumwaminisha kila mtoto wa Mungu kwamba ni mapenzi ya Mungu yeeye apokee Roho Mtakatifu.

Mstari huo huo pia unathibitisha ukweli kwamba kubatizwa kwa Roho Mtakatifu hutokea baada ya wokovu, kwa sababu hapa Yesu aliiwaahidi watoto wa Mungu (watu pekee amba Mungu ndiye “Baba yao wa mbinguni”) kwamba angewapa Roho Mtakatifu, wakiomba. Bila shaka ni kwamba, kama ujuzi pekee na Roho Mtakatifu amba mtu angepata ni kuzaliwa mara ya pili wakati wa wokovu tu, basi ahadi ya Yesu isingekuwa na maana. Kinyume na kikundi cha wanatheolojia wachache wa kisasa ambacho kinaelekeea kutoweka, Yesu aliamini kwamba ni sawa kabisa kwa watu waliokwisha zaliwa mara ya pili kumwomba Mungu awape Roho Mtakatifu.

Kwa maneno ya Yesu, kuna masharti mawili tu ambayo lazima mtu atimize ikiwa anataka kupokea Roho Mtakatifu. Kwanza – Mungu lazima awe Baba, na ndivyo ilivyo kama umezaliwa mara ya pili. Pili – umwombe Roho Mtakatifu.

Pamoja na kwamba kumpokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ni kitu kinachoungwa mkono na Maandiko (ona Matendo 8:17; 19:6), si lazima. Mkristo yejote anaweza kumpokea Roho Mtakatifu akiwa peke yake katika faragha yake ya maombi. Anachohitaji kufanya ni kuomba tu, kupokea kwa imani, na kuanza kunena kwa lugha kama Roho atakavyomwezesha kutamka.

Hofu Za Wengi

Kuna watu wenye kuogopa kwamba wakiomba Roho Mtakatifu, wanaweza kujiweka wazi kuingiwa na pepo. Hakuna msingi wowote wa hofu kama hiyo. Yesu aliahidi hivi:

Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanamwe akimwomba
mkate atampa jiwe, au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au
akiomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa

watoto wenu vipawa vyema, je! Baba yenu wa mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao? (Luka 11:11-13).

Tukiomba Roho Mtakatifu, Mungu atatupa Roho Mtakatifu. Tusiwe na hofu kwamba tutapokea kitu kingine chochote!

Kuna wengine wenyewe kuogopa kwamba, wakinena kwa lugha, ni kitu chao watakachokuwa wametunga badala ya lugha ya kimujiza itolewayo na Roho Mtakatifu. Sawa – ila, kama utajaribu kutunga lugha ya hakika kabla ya kubatizwa na Roho Mtakatifu utagundua kwamba ni kitu kigumu sana, kisichowezekana. Ila, ni lazima uelewe kwamba kama utanena kwa lugha nyingine, itakubidi utumie midomo yako, ulimi, na ngano za sauti. Roho Mtakatifu hakusemei – anakupa lugha. Yeye ni *msaidizi* wetu, si *anayetenda*. Inakupasa *wewe* useme. Ni kama Biblia inavyofundisha, kwamba:

Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, *kama Roho alivyowajalia kutamka* (Matendo 2:4 – Maneno mepesi kutilia mkazo).

Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; *wakaanza* kunena kwa lugha (Matendo 19:6 – Maneno mepesi kutilia mkazo).

Baada ya mwamini kuomba zawadi ya Roho Mtakatifu, anatakiwa kuamini na kutazamia kunena kwa lugha nyingine. Kwa kuwa Roho Mtakatifu anapokelewa kwa imani, mwenye kupokea asitazamie hisia za namna fulani au msisimko kimwili. Anatakiwa kufungua kinywa chake tu na kuanza kutamka zile sauti mpya na silabi zitakazosababisha ile lugha mpya ambayo Roho Mtakatifu anampa. Mwamini asipoanza *kusema kwa imani*, hakuna maneno yatakayotokea kinywani mwake. Ni lazima *yeye* aseme, ndipo Roho Mtakatifu atakapomjalia kutamka.

Mahali Lugha Inapotoka

Kulingana na Paulo – aaminiye anapoomba kwa lugha – si akili yake iombayo bali ni roho yake.

Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda. Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia, nitaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia (1Wakor. 14:14-15).

Paulo alisema kwamba alipoomba kwa lugha, akili yake haikuwa na matunda. Maana yake ni kwamba akili yake ilikuwa haihusiki, wala hakuelewa alichokuwa anaomba kwa lugha. Basi, anachosema ni kwamba, badala ya kuomba kwa lugha wakati wote na huku haelewi anachosema, aliquwa pia anaomba kwa akili, kwa lugha yake mwenyewe. Alitumia muda mwingi kuimba kwa lugha na kuimba kwa akili yake pia. Ipo nafasi kwa maombi ya aina zote hizo mbili pamoja na kuimba kwa aina zote hizo mbili, nasi tuwe na busara kufuata mfano wa Paulo.

Ona pia kwamba, kwa Paulo, kunena kwa lugha kulikuwa chini ya mamlaka ya mapenzi yake, sawa na jinsi kuzungumza lugha yake kulivyokuwa. Alisema hivi: “Nitaomba kwa roho na nitaomba kwa akili pia” (TLR). Mara nyingi wakosoaji hudai kwamba kama kunena kwa lugha siku hizi ni zawadi kweli kutoka kwa Mungu, hakuna mtu ambaye angeweza kuitawala, maana kufanya hivyo ni sawa na kumtawala Mungu. Wazo kama hilo halina msingi wowote. Kunena kwa lugha zamani na siku hizi kuko chini ya mamlaka ya mtu binafsi, na ndivyo Mungu alivyopanga. Wakosoaji hao ni vizuri waendelee na kusema kwamba watu wenye mikono ambayo imeumbwa na Mungu *kweli* hawana mamlaka na utawala juu ya mikono yao, na watu wenye kufanya maamuzi ya kutumia mikono yao wanamtawala Mungu.

Ukisha batizwa kwa Roho Mtakatifu, ni rahisi sana kuthibitisha kwamba kunena kwa lugha kwako kunatoka rohoni na si akilini mwako. Kwanza – Hebu jaribu kuzungumza na mtu huku unasoma kitabu hiki. Utaona kwamba huwezi kufanya yote mawili kwa wakati mmoja. Lakini, utagundua kwamba unaweza kuendelea kunena kwa lugha unapoendelea kusoma hiki kitabu. Sababu ni hii: hutumii akili yako kunena kwa lugha – tendo la kunena hutoka rohoni mwako. Basi, unapotumia roho yako kuomba, waweza pia kutumia akili yako kusoma na kuelewa.

Sasa – Kwa Kuwa Umebatizwa Kwa Roho Mtakatifu

Usisahau sababu kuu ya Mungu kukupa ubatizo wa Roho Mtakatifu – ni ili kukutia nguvu kwa ajili ya kuwa shaiidi Wake, kwa madhihirisho ya tunda na karama (au zawadi) za Roho Mtakatifu (ona 1Wakor. 12:4-11; Wagal. 5:22-23). Unapoishi maisha yanayofanana na Kristo na kujonesha upendo Wake, furaha na amani Yake kwa dunia pamoja na kudhihirisha karama zisizo za kawaida za Roho, Mungu atakutumia kuwavuta wengine Kwake. Uwezo wa kunena kwa lugha ni sehemu moja tu ya “mito ya maji yaliyo hai” inayotakiwa kububujika kutoka ndani mwako.

Pia kumbuka kwamba Mungu alitupa Roho Mtakatifu atuwezeshe kuwafikishia Injili watu *wote* duniani (ona Matendo 1:8). Tunaponena kwa lugha zingine, tunapaswa pia kutambua kwamba lugha tunayosema inaweza kuwa lugha ya kabilia fulani au nchi fulani ya kigeni. Kila mara tunapoomba kwa lugha, tukumbuke kwamba Mungu anataka watu wa kila lugha wasikie habari za Yesu. Tunapaswa kumwomba Bwana kuhusu jinsi anavyotaka sisi tuhusike kutimiza Agizo Kuu la Yesu Kristo.

Kunena kwa lugha ni kitu tunachopaswa kufanya mara nyingi iwezekanavyo. Paulo – mtu wa hali ya juu sana kiroho – aliandika hivi: “Ninamshukuru Mungu kwamba mimi nanena kw alugha zaidi yenu wote” (1Wakor. 14:18, TLR). Aliandika maneno hayo kwa kanisa lililokuwa linanena sana kwa lugha (japo kwa nyakati zisizofaa). Basi, Paulo bila shaka alinena kwa lugha mara nyingi sana mpaka akawazidi. Kuomba kwa lugha hutusaidia kumtambua Roho Mtakatifu anayeishi ndani yetu, na itatusaidia “kuomba bila kukoma” kama Paulo alivyofundisha katika 1Wathes. 5:17.

Vile vile Paulo alifundisha kwamba kunena kwa lugha zingine humjenga mwamini (ona 1Wakor. 14:4). Maana yake ni kwamba inatujenga kiroho. Kwa kuomba kwa lugha, tunatia nguvu utu wetu wa ndani kwa njia tusizoelewa kabisa. Kunena kwa lugha kunatakiwa kuleta utajiri mpya kila siku katika maisha ya kiroho ya kila aaminiye, wala si tukio la wakati mmoja tu tunapojazwa na Roho Mtakatifu mara ya kwanza.

Ukiisha batizwa kwa Roho Mtakatifu, ninakutia moyo utumie muda mwingi kila siku kumwomba Mungu kwa lugha yako mpya. Itakusaidia sana katika maisha yako ya kiroho na kukua kwako kiroho.

Majibu Kwa Maswali Kadhaa Ya Kawaida

Je, tunaweza kuwa na uhakika kabisa kwamba wote ambao hawajawahi kunena kwa lugha hawajabatizwa na Roho Mtakatifu? Mimi nadhani sivyo.

Sikuzote nimewatia watu moyo watazamie kunena kwa lugha wakati nilipowaombea kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, nami nadhani asilimia 95 ya hao walifanya hivyo baada ya kuwaombea kwa nukta chache. Ni maelfu ya watu kwa kipindi cha miaka mingi sana.

Lakini siwezi kusema kwamba Mkristo aliyeomba kubatizwa kwa Roho na ambaye hajanena kwa lugha hajabatizwa na Roho Mtakatifu. Hii ni kwa sababu ubatizo wa Roho hypokelewa kwa imani, na kunena kwa lugha ni kitu cha hiari. Ila, nipatapo nafasi ya kuzungumza na mwamini ambaye ameomba kubatizwa na Roho Mtakatifu lakini hajawahi kunena kwa lugha, ninachoanza nacho ni kumwonyesha mtu huyo maandiko yote katika kitabu cha Matendo kuhusu swala lenyewe. Isha, ninamwonyesha huyo mwamini jinsi ambavyo Paulo aliandika, kwamba yeze husimamia wakati wa kunena na wakati wa kutonena kwa lugha. Kama Paulo, mimi mwenyewe naweza kunena kwa lugha wakati wowote ninaotaka, na hivyo naweza kuamua, nikitaka, kutonena tena kwa lugha. Kama ni hivyo, inawezekana nikawa nimebatizwa kwa Roho Mtakatifu na kutonena kwa lugha kwa kutoshirikiana na tamko analoleta Roho Mtakatifu.

Basi – ninapokuwa na nafasi ya kuzungumza na Mkristo ambaye ameomba kwa imani apooke ubatizo wa Roho Mtakatifu lakini hajawahi kunena kwa lugha, simwambii jinsi ambavyo kunena kwa lugha si kitu Roho anachofanya bila sisi. Ninajaribu kumweleza kwamba Roho Mtakatifu ndiye ajaliaye kutamka, lakini sisi lazima tuseme – au tunene – sawa tu na jinsi ambavyo inakuwa mtu anaposema lugha ya kawaida. Kisha ninamtia moyo mtu huyo kushirikiana na Roho Mtakatifu na kuanza kunena kwa lugha. Mara nyingi baada ya hayo, watu hao hunena baadaye.

Je, Paulo Hakuandika Kwamba Si Wote Wanenao Kwa Lugha?

Swali la Paulo – “Kwani ni wote wanenao kwa lugha?” (1Wakor. 12:30) – ambalo jibu lake dhahiri ni “Hapana” lazima litazamwe kwa kuangalia Agano Jipyka kwa jumla. Swali lake linapatikana katika mantiki ya mafundisho aliyotoa juu ya karama za kiroho, ambazo zinadhahirishwa kadiri Roho apendavyo tu (1Wakor. 12:11). Paulo alikuwa anaandika kuhusu karama ile ya “aina za lugha” (1Wakor. 12:10), ambayo, kulingana na Paulo, lazima kila mara iambatane na karama ya kiroho ya tafsiri za lugha. Hii karama isingweza kuwa ile ambayo Wakorintho waliitumia mara kwa mara kanisani mwao, kwa sababu wao walikuwa wanenao kwa lugha hadharani pasipo kuwepo na mtu wa kutafsiri. Tunatakiwa kujuiliza hivi: *Kwa nini Roho Mtakatifu atoe karama ya lugha kwa mtu katika ibada ya hadhara, bila ya kumpa mtu mwengine karama ya kutafsiri?* Jibu ni kwamba hawezo kufanya hivyo, maana akifanya, hawi anaendeleza mapenzi ya Mungu.

Bila shaka Wakorinto walikuwa *wanaomba* kwa lugha kwa sauti wakati wa ibada zao kanisani bila ya kuwepo na tafsiri aina yoyote. Basi, tunajifunza kwamba kunena kwa lugha kuna matumizi mawili tofauti. Moja ni kuomba katika lugha, ambako Paulo

anasema kufanywe kibinafsi. Matumizi hayo hayaambatani na tafsiri, kama Paulo alivyoandika, kwamba, “Roho yangu huomba, lakini akili yangu haina matunda” (1Wakor. 14:14). Ni kwamba Paulo hakujuua kila wakati alikuwa anasema nini aliponena kwa lugha. Hakuelewa, wala haikuwepo tafsiri.

Ila pia kuna matumizi ya kunena kwa lugha ambayo ni kwa ajili ya kusanyiko, na hayo huambatana na karama ya tafsiri ya lugha. Hiyo hutokea wakati Roho Mtakatifu anapomjia mtu fulani kama apendavyo, akimpa karama hiyo. Mtu huyo atanena waziwazi, kisha inakuwepo tafsiri. Ila, Mungu hamtumii kila mtu hivyo. Ndiyo sababu Paulo aliandika kwamba si wote wanenao kwa lugha. Si wote wanaotumiwana Mungu katika kile kipawa kitolewacho mara moja cha lugha, kama ambavyo Mungu hamtumii kila mtu katika karama ya tafsiri za lugha. Hiyo tu ndiyo njia rahisi ya kufafanua swali la Paulo – “Kwani ni wote wanenao kwa lugha?” – na yanayofundishwa na Maandiko kwa ujumla.

Mimi naweza kunena kwa lugha wakati wowote nitakao, kama na Paulo pia. Basi, hatuwezi kusema kwamba kila tunaponena kwa lugha, ni “kama Roho apendavyo tu.” Hapana – ni kama *sisi* tupendavyo. Kwa hiyo, tunachofanya kila tunapotamani *si* karama ya kunena kwa lugha itokeayo “kama Roho apendavyo tu.” Tena, Paulo – kama mimi – alinena kwa lugha kibinafsi pasipo kuelewa alichokuwa anasema. Basi, hiyo *si* karama ya lugha ambayo aliandika habari zake katika 1Wakorintho, aliyosema kwamba lazima kila mara iambatane na karama ya tafsiri ya lugha.

Ni mara chache sana nimenena kwa lugha katika kusanyiko. Ni wakati nilipojisikia kwamba Roho Mtakatifu amenishukia ili nifanye hivyo, japo ningeweza (kama Wakorintho walivyokuwa wanafanya) kuomba kwa lugha kwa sauti wakati wowote niliotaka nikiwa kanisani bila ya kuwepo tafsiri. Ninapohisi Roho Mtakatifu akinijilia kwa nguvu na karama hiyo, kila mara imekuwepo tafsiri ambayo ililetu kujengwa kwa mwili wa Kristo wakati huo.

Tunapohitimisha sehemu hii, ni vizuri kutafsiri Biblia kwa umoja. Wale wanaosema kwamba si waamini wote wanaopaswa kunena kwa lugha kwa sababu ya swali la Paulo katika 1Wakorinto 12:30, wanapuuza maandiko mengine mengi sana yasiyokubaliana na tafsiri yao. Kwa sababu ya kosa lao, wanakosa baraka kubwa sana kutoka kwa Mungu.